

MIENENDO MIPYA KATIKA UANDISHI WA KEZILAHABI: NAGONA NA MZINGILE

Mwenda Mbatiah

Utangulizi

Riwaya ya Kiswahili imepiga hatua kubwa za maendeleo, hasa katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita kufikia sasa. Kwa hivyo Topan (1982:127) anaposema kuwa riwaya hiyo imekwisha kupita utoto wake anatoa maoni yanayokubalika miongoni mwa wahakiki wengi. Topan anaendelea kudai kuwa watunzi muhimu zaidi wa riwaya ya Kiswahili ni M.S. Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Hiyo pia ni kauli muhimu ingawa wanariwaya wapevu wa Kiswahili ni wengi kuliko hao wawili waliotajwa.

Katika makala haya tunazihakiki kazi za kinathari za Kezilahabi kwa kutilia maanani umuhimu wa mwandishi huyu katika kuipavusha riwaya ya Kiswahili. Katika tahakiki hii lengo letu kuu litakuwa ni kuthibitisha kwamba baada ya kuchapishwa *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), uandishi wa Kezilahabi umeingia katika mkondo mpya. Kama tutakavyoonyesha katika makala haya, kazi hizo mbili zinatofautiana na kazi za awali kwa njia kadhaa. Swali linalozuka katika hali hii ni kwamba je, *Nagona* na *Mzingile* zinawakilisha hatua gani katika uandishi wa Kezilahabi, na hatua yenyewe ni ya kwenda mbele au ni ya kurudi nyuma? Tutalishughulikia swali hili. Uandishi wa Kezilahabi unagawika mara mbili kama ifuatavyo: (i) Kazi za kipindi cha kwanza ambazo ni *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Gamba la Nyoka* (1979). Mbali na riwaya hizo, Kezilahabi pia ameandika hadithi fupi kama vile "Cha Mnyonge Utakitapika Hadharani" "Wasubiri Kifo" na nyinginezo.¹ (ii) Kazi za kipindi cha pili ambazo ni *Nagona* na *Mzingile*. Makala haya yatabainisha misingi ya uainishaji huu.

Kipindi cha Kwanza

Kezilahabi alijitambulisha kama mwandishi stadi wa riwaya wakati kazi yake ya kwanza, *Rosa Mistika* ilipotoka, akiwa bado ni mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wazo kuu analolikuza katika riwaya hii ni kwamba tabia na mwenendo wa wanadamu huumbwa na mazingira yake ya kijamii. Hivyo basi iwapo mazingira hayo ni mabaya, hayawezi kumzaa mwanadamu aliyekamilika kiutu. Wazo hili linakuzwa kupitia mhusika mkuu, Rosa. Mwandishi anayafuata maisha ya Rosa tangu akiwa msichana mdogo wa kijijini, chini ya ulinzi mkali wa babake ambaye ni mlevi. Malezi ambayo Rosa anayapata nyumbani hayamtayarishi kwa maisha yake ya baadaye. Akiwa nyumbani babake Zakaria anamkataza kabisa kushirikiana na wanaume. Anapotoka nyumbani na

kwenda shuleni anakuta kuwa ulimwengu pia unao wanaume, wanaomtaka kwa mapenzi. Kwa kuwa hakutayarishwa kuishi na viumbe kama hao, anatumbukia katika bahari iliyoachafuka ya mapenzi bila kujua kuiogelea. Tunaelezwa kuhusu maisha yake anapokuwa katika shule ya bwani ya Rosary kuwa:

Rosa sasa alianza mapenzi. Alianza mapenzi lakini aliyaandea haraka sana kama mbwa aliyekata kamba. Aliona mvulana mmoja au wawili hawamtoshi kwa urafiki. Mwaka huo huo aliwakubali wavulana watano (uk.42).

Kutoka shule ya Rosary, Rosa anakwenda Morogoro TTC, na hatimaye anahitimu kuwa mwalimu. Lakini sasa bahari ya mapenzi imemshinda kuogelea. Anaanza kuzama. Maisha ya kufanya mapenzi ovyoovyo yamekwisha kumpiga dhoruba kali sana. Hatimaye anaona kuwa ndoa ndiyo inayoweza kumletea utulivu maishani. Lakini Charles Lusato, mchumba wake, anapofichuliwa maisha ya umalaya ya Rosa katika siku za nyuma, anamkataa. Pigo hili ndilo linalommaliza Rosa, na anajiua.

Hisia inayotawala katika riwaya hii ni ya kicheko cha uchungu. Mwandishi anaicheka jamii yake kwa kushindwa kuwalea watoto wake wa kike. Juhudi zinazofanywa na asasi mbalimbali za kijamii kuhusu jukumu hili la malezi ni za kuchekesha. Katika kiwango cha familia tumeona kuwa baba anaamini kuwa kuwachunga watoto wa kike ili wasichanganyike na wenzao wa kiume, ndiyo malezi bora. Uchungaji huu unazidi pale ambapo watoto hao wanakwenda shuleni. Shule anaposomea Flora, mdogo wake Rosa, inalindwa hata na askari. Flora anamwambia nduguye: "Rosa, shule yetu hii ni ya ajabu. Tunalindwa kama watoto wadogo..." (uk. 75). Malezi haya mabovu yanakiangamiza kizazi kizima cha watoto wa kike. *Rosa Mistika* ni riwaya ya kijamii inayochimbuka kutokana na uhalisi wa mazingira mahususi ya kijamii. Mulokozi anaifungamanisha na jamii kwa kubainisha uhusiano wake na maisha ya mwandishi mwenyewe, ambaye ni zao la jamii. Anasema: "Kuandika riwaya hiyo kulikuwa ni namna ya uasi wa maisha ya kisufii ya kuandaliwa kuwa padre."²

Katika riwaya ya pili - *Kichwamaji*, tunamuona Kezilahabi akiyachambua maisha ya jamii yake, kwa kugemea falsafa ya udhanaishi (*existentialism*). Hii ni falsafa inayotilia maanani sana tajiriba za mtu binafsi katika safari yake ya maisha. Katika mataifa ya Ulaya, falsafa hii ilijitokeza katika fasihi baada ya Vita Vikuu vya Pili, ambapo waandishi kama J.P. Sartre, Samuel Beckett, Albert Camus na wengineo walijitokeza na kazi zilizobobea katika falsafa hii. Fasihi iliyotokana na tapo hilo la waandishi ilikuja kujulikana (kwa Kiingereza) kama "*Literature of the Absurd*." Kwa ujumla, fasihi hii inatilia mkazo unasibu (*arbitrariness*) na uduni (*absurdity*) wa maisha ya mwanadamu. Kwa hali hii, fasihi ya aina hii inaweza kufasiriwa kwa Kiswahili kama "fasihi ya uduni". Inasawiri picha ya mwanadamu kama kiumbe dhaifu kinachoishi maisha yasiyo na maana katika ulimwengu usio na maana.

Katika *Kichwamaji* mtazamo huu unajitokeza kupitia kwa mhusika mkuu, Kazimoto. Mwandishi ameitumia sana mbinu ya uzungumzi nafsia kutufichulia mawazo ya Kazimoto, ambaye ndiye msimulizi, kuhusu dhana kama vile kifo, furaha, maisha, na Mungu. Kazimoto ambaye haamini kuna kitu kama Mungu, anayaona maisha kama adhabu. Anasema "Niliona kuwa adhabu kubwa ya mwanadamu ni maisha yenyewe" (uk.94).

Ingawa *Kichwamaji* inajishughulisha na masuala ya kifalsafa yaliyotajwa, bado imejikita katika jamii mahsusi. Matatizo ya jamii hiyo na mustakabali wake, ndiyo mambo yanayopewa uzito zaidi na mwandishi. Kwa kifupi, maudhui ya riwaya hii ni kwamba kizazi cha vijana waliopata elimu ya juu hakina matumaini ya kufaulu maishani au kuiendeleza jamii, kwa sababu, kwanza, kimekengeushwa na elimu ya Kimagharibi, na pili, kimeharibiwa na uoza ulioletwa na mabadiliko ya kijamii, ambapo mfumo wa kimaadili wa kijadi umemomonyoka. Kazimoto na rafiki yake Manase, wamekiambukiza kizazi chao ugonjwa wa zinaa waliopata kwa Pili. Vichwa vikubwa vya watoto wanaowazaa vinaonyesha kwamba watakuwa kama wazazi wao ambao ni vichwamaji. *Kichwamaji* ni ishara ya ukosefu wa mawazo muafaka katika muktadha wa jamii. Hivyo basi, ni alama ya mkengeuko.

Hatimaye, Kezilahabi anasema kwamba kizazi cha vibwanyenye waliopata elimu ya juu waishio mijini, hakiwezi kutegemewa katika ujenzi wa jamii mpya ya Tanzania baada ya uhuru. Msingi wa jamii mpya ni katika sehemu za mashambani wanakoishi watu wa kawaida na wakulima kama Kabenga, babake Manase, na Mafuru, babake Kazimoto. Familia za wazee hawa zinashirikiana kulima shamba kubwa la pamoja, na matokeo yake yanakuwa mazuri sana. Hii ni ishara ya mafanikio ya siasa ya ujamaa, ambayo dalili za mwanzo wake zinaonekana.

Kwa kiwango fulani riwaya *Dunia Uwanja wa Fujo* inaendeleza mjadala kuhusu tatizo la maisha unaoanza katika *Kichwamaji*. Kama kichwa cha riwaya yenyewe kinavyodokeza, wazo analolikuza mwandishi ni kwa maisha ya mwanadamu ni vurumai ambayo huletwa ulimwenguni na watu fulani katika nyakati mbalimbali za kihistoria. Hatimaye vurumai hizo hazina maana yoyote kwa sababu hufifia baada ya muda na nyingine kuzuka. Dhana ya uduni wa mwanadamu inayojitokeza katika *Kichwamaji* inaendelezwa zaidi katika riwaya hii. Mwandishi anatupa taswira ya mwanadamu kama kiumbe dhaifu kisichoweza kuudhibiti ulimwengu, kuufanya ukitumikie na ulete furaha katika maisha yake. Kwa hali hii juhudi zozote anazofanya mwanadamu ili apate furaha zinashindwa.

Falsafa ya maisha anayoishughulikia mwandishi imekitwa kwenye mazingira mahsusi ya kihistoria, yaani Tanzania baada ya Azimio la Arusha. Kutangazwa kwa Azimio mwaka wa 1967 ni tukio lililoleta mabadiliko makubwa katika jamii nzima ya Tanzania. Mabadiliko hayo yaliwaathiri watu binafsi na mara nyingine kuleta migogoro mikubwa katika maisha yao. Maisha ya Tumaini,

mhusika mkuu wa riwaya hii, yanathibitisha jambo hili. Maangamizo ya Tumaini yanatokana na upinzani wake dhidi ya sera za Azimio. Kushindwa kwake kunaashiria kushinda kwa siasa ya ujamaa.

Utekelezaji wa sera za Azimio la Arusha na siasa ya ujamaa unashughulikiwa kikamilifu katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*. Hii ni riwaya ya kisiasa. Kezilahabi anatumia mtindo wa tashtiti, kama alivyofanya Achebe katika riwaya yake: *Mwakilishi wa Watu*. Kama Achebe anavyoicheka siasa mbovu ya Nigeria na kuwabeza viongozi wake wakora kama Mtemi Nanga, ndivyo Kezilahabi anavyoicheka siasa ya ujamaa na kuwabeza wahubiri wake ambao ni viongozi wapotovu kama Mamboleo na Mambosasa. Mwandishi anaonyesha kwamba ujamaa ulielekea kushindwa kwa sababu ya udhaifu wa kibinafsi wa viongozi na kwa sababu ya matatizo ya kiutendaji ya kutekeleza maazimio ya ujamaa. Mkinzano mkuu wa siasa ya ujamaa ni kwamba maoni ya wananchi hayakutiliwa maanani wakati wa kubuniwa sera zake. Mamboleo anasema, "Lakini watu hawakuanzisha wazo la ujamaa. Wazo hili limetoka juu na kuwaangukia watu kama jiwe walibebe." (uk. 51). Katika hali kama hii haishangazi kwamba wananchi wanakataa kubebeshwa mzigo wa ujamaa, ambao hawaoni maana yake. Mulokozi (1983:5) akiliangalia tukio la majilio ya ujamaa katika darubini ya kiMarx, anatoa rai inayoangaza kiini cha mgogoro ulioikumba siasa hiyo. Anasema, tatizo la ujamaa lilikuwa hasa ni ubatili wake. Yaani viongozi walijaribu kuupa umma wa Tanzania zawadi ya ujamaa wakati umma wenyewe haukuwa umeiva kuanzisha vita vya kitabaka. Kwa mujibu wa nadharia ya Marx, vita vya kitabaka ndiyo njia ya pekee ya kuleta usoshalisti wa kweli.

Ujamaa nchini Tanzania ni mojawapo katika majaribio ya kisiasa ya masafa mafupi yaliyoanzishwa na viongozi wengi wa Kiafrika baada ya uhuru. Ingawa ubeberu ulichangia katika kushindwa kwa majaribio hayo, viongozi walioyaanzisha wanalaumika kwa sababu kwanza, hawakufanya maandalizi ya kutosha, na pili, walijaribu kutumia njia ya mkato na kufanya mambo kwa pupa ili kuleta mabadiliko makubwa ya kijamii wakati wa uhai wao. Matokeo yake ni maangamizo makubwa ya watu wa kawaida tunayoyaona katika *Gamba la Nyoka*.

Kazi nyingine ya Kezilahabi inayoshambulia ujambazi wa kisiasa ni hadithi yake iliyotia fora, "Wasubiri Kifo". Katika hadithi hii, kicheko cha mwandishi kimeelekezwa katika unyonge ambao wananchi wamepatiwa na viongozi wao. Wanasiasa wanawadanganya kwamba Azimio la Arusha litaleta mabadiliko na maisha bora zaidi kwao. Lakini hakuna mazuri yanayotokea. Wanabakia maskini wakisubiri kifo, huku viongozi wao wakiendelea kujitajirisha.

Kufikia hapa tumeziangalia kazi za kinathari za Kezilahabi katika kipindi cha kwanza cha uandishi wake. Kinachojitokeza wazi ni kwamba kuna sifa nyingi za kimaudhui na kimtindo zinazolingana katika kazi hizo, na hivyo kuzifanya zizeze kuchukulika kama mkondo mahsusi wa kisanaa. Kimaudhui, kazi hizo

zinayajadili masuala ya kifalsafa na ya kimalimwengu, kwa kuyaegemeza swali la maana ya maisha. Mwelekeo wa kifalsafa wa mwandishi ni wa kiudhanaishi. Kwa kuongozwa na falsafa hii, anaelekea kutoona thamani ya mwanadamu na maana ya maisha yake. Hata hivyo, muhimu zaidi ni kwamba kazi hizo ni za kiuhalisia kwa kuwa zinafuata maendeleo ya kijamii ya Tanzania ya kisasa, tangu uhuru hadi baada ya Azimio la Arusha. Kwa hivyo ni kazi za kijamii zinazomulika hali halisi ya watu katika jamii. Tunasisitiza kwamba ingawa mwandishi anatumia darubini ya kukatisha tamaa ya udhanaishi katika uchambuzi wake wa jamii, hatimaye anaonyesha kwamba kuna matumaini. Riwaya kama *Gamba la Nyoka* inaashiria waziwazi kufaulu kwa ujamaa. Kwa ujumla basi, matumaini ya mwandishi yamo kwenye utamaduni wa kijadi wa Mwafrika na kwenye falsafa ya ujamaa ambayo ilitokana na utamaduni huo.

Mtindo wa mwandishi ndio unaozileta pamoja zaidi kazi za kipindi cha kwanza. Mawazo ya mwandishi yamewasilishwa kwa lugha ambayo Kitsao ameleza kama lugha ya kimaongezi na inayokwenda haraka.³ Lugha ya Kezilahabi ni ya kulisimua na iliyojaa ucheshi. Kwa sababu hii, mtindo wake wa kitashtiti umefanikiwa. Tashtiti zake zina uwezo mkubwa wa kuathiri ipasavyo. Tunacheka tukisoma, lakini tunajicheka wenyewe kwa sababu uoza unaobainishwa ni uoza na udhaifu wa jamii zetu. Masimulizi ya kazi hizo yamejaa tamathali, hasa sitiari, tashbihi, nahau na methali za Kikerewe. Hali hii inaipa lugha yake sifa ya upya na muonjo wa utamaduni wa Kiafrika.

Kipindi cha Pili

Katika muktadha wa uandishi wa kinathari katika Kiswahili, *Nagona* na *Mzingile* zinajitokeza kama kazi za kimajaribio. Kwa sababu hii, haziainishiki kwa urahisi chini ya tanzu za kijadi kama riwaya, hadithi fupi na novela. Mlacha na Madumulla (1991:24-25) wanaieleza *Nagona* kuwa ni riwaya, na kuendelea kusema kwamba inalingana kimtindo na kimaudhui na riwaya ya Christa Wolf iitwayo *Cassandra*. Kuchukulia kwamba kazi hiyo ni riwaya kunaelekea kukinzana na fasili ya riwaya wanayoitoa. Wanasema, "Riwaya ni hadithi iliyotungwa ambayo ina urefu wa kutosha, visa vinavyoana na ambayo inazingatia suala la muda."⁴ *Nagona* na hata *Mzingile*, hazioani na maelezo hayo, kama makala haya yatakavyobainisha. Hatuna dhamira ya kujadili kwa kirefu suala la fasili ya riwaya kwa kuwa limejadiliwa vya kutosha na wataalamu kama Forster (1927:24-27), Boulton (1975:I-14), na wengineo. Aidha, makala haya hayana nafasi ya kushughulikia kikamilifu suala la riwaya ya Kiswahili, au uainishaji wa tanzu za kinathari katika Kiswahili. Hata hivyo tunaonelea kwamba *Nagona* na *Mzingile* zinakaribiana zaidi na utanzu wa novela kuliko vile zinavyokaribiana na utanzu wa riwaya.⁵ Lakini tunasisitiza kwa kimtindo na kimaudhui, hizi ni kazi za kimajaribio. Hivi si kusema kwamba ni za kiwango cha chini.

Nagona na *Mzingile* hazina mtiririko wa matukio ambayo msomaji anaweza kuyafuata tangu mwanzo hadi mwisho. Kazi hizo zinajitokeza kama masimulizi ya visa vya kiajabuajabu ambavyo havikushikamanishwa na uzi mmoja wa kiploti. Masimulizi yenyewe hayana urefu wa kutosha wa kutungia riwaya. Urefu wa *Nagona* ni kurasa 62 na ule wa *Mzingile* ni kurasa 70. Vipengele vya kimsingi vya riwaya kama ukuzaji wa wahusika na usawirishaji wa mandhari halisia hazipo katika kazi hizo. Aghalabu mandhari ya masimulizi hayana sura ya ulimwengu tunaoufahamu, bali ni ya kuzimuni. Istitoshe, masimulizi hayo hayakukitwa kwenye mazingira mahsusi ya kijamii na kiwakati. Hivi ni tofauti kabisa na riwaya za kipindi cha kwanza cha uandishi wa Kezilahabi. Kwa ujumla, kazi mbili tunazozitungumzia si za kiuhalisia. Hivyo basi kuziita "riwaya" ambayo hujitambulisha kwa mtindo wake wa kiuhalisia, ni kupurukusha maana ya dhana na istilahi za kifasihi.

Kwa kutumia visa visivyokuwa na mpangilio wowote, mwandishi anatoa tafsili yake ya hadithi ya mwanadamu katika ulimwengu. Wazo kuu analochunguza ni lile la kuwepo kwa mwanadamu ulimwenguni. Anajaribu kutanzua kitendawili cha maana ya maisha ya mwanadamu, nafasi yake ulimwenguni, asili yake na hatima yake. Ni kweli kwamba kwa kiwango fulani mambo haya yanajitokeza katika kazi za kipindi cha kwanza, hasa riwaya za *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo*. Hata hivyo, *Nagona* na *Mzingile* zinajikita kabisa katika masuala hayo ya kidhanaishi, bila kujishughulisha na masuala ya kijamii, ambayo kama tulivyoona, ndiyo mhimili wa riwaya zote za awali alizozitunga Kezilahabi. Madumulla (1991:25) anasema kuhusu *Nagona* kwamba, "Kwa namna fulani riwaya hii ina mhusika wa kidhanaishi, na riwaya yenyewe ni hatua ya juu kabisa ya riwaya kidhanaishi." Tukipuuza matumizi ya neno "riwaya", matamshi hayo ni muafaka, na yanafaa kuieleza hata novela ya *Mzingile*.

Katika kuyashughulikia masuala ya kidhanaishi na kifalsafa yaliyotajwa, mwandishi ametumia mtindo wa kitaashira na kisitiari. Vipengele vikuu vya novela hizo mbili, kama wahusika, visa na mandhari, ni vya kikale na kivisaasili. Hivyo basi maana ya kazi hizo inaweza tu kupatikana kwa kutalii na kufasiri visaasili, vikale na tamathali nyingi zilizotumiwa.

Katika *Nagona*, sauti inayotoa masimulizi ni ya mhusika mkuu. Masimulizi yake ni kumbukumbu za maisha yake ya siku za nyuma, pamoja na ndoto zake. Mwishoni mwa sura ya saba anasema, "Yote haya yalitokea zamani nilipokuwa bado mtoto. Nilikuwa na umri wa miaka kumi na minne alipofariki babu" (uk. 46). Sehemu inayohusika na maisha hasa ya msimulizi ni ndogo sana ikiilinganishwa na ile inayochukuliwa na ndoto zake. Kuhusu maisha yake, msimulizi anaeleza jinsi babu yake alivyozoea kumwambia ajiandae kuwa msakaji wa ukweli. Aliusiwa, "Usiwe na haraka. Kuna vikwazo vingi, lakini kushinda vikwazo si kufikia kweli, Safari ni ndefu lakini kusafiri si kufika" (uk. 24).

Maneno haya yanadokeza kwamba safari anayoifanya msimulizi baada ya kifo cha babu yake ni safari ya kifikra. Yaani ni juhudi zake za kimawazo za kuyatalii maisha na ulimwengu, ili kutanzua kitendawili cha kuwepo kwake ulimwenguni, na hatima ya maisha yake. Wasia wa babu yake ni kwamba ishara itakayomwambia lini aianze safari ni "Siku ya ajali katika bonde la taaluma" (uk. 45). Motifu ya ajali inajitokeza sana katika kazi hii. Matukio yake muhimu katika maisha ya mwanadamu ni matokeo ya ajali. Motifu hii inatilia mkazo unasaibu wa maisha na uduni wake. Ajali itakayoashiria wakati wa masimulizi kuanza safari yake, inaelekea kuwa ni ile ajali ya ndege inayoelezwa katika sura ya nne. Yamkini ndege inaanguka kutokana na hali mbaya ya anga, ambapo msimulizi anakufa. Hata hivyo kifo chake hakielezwi waziwazi. Tunadokezewa kwamba hali yake imebadilika. Wazo tunalowasilishiwa hapa ni kwamba hakuna mpaka thabiti baina ya uhai na kifo. Wazo hili linatawala kazi nzima hivi kwamba, katika masimulizi hatuwezi kupambanua baina ya mazingira ya ufu na uhai. Hivi ni kusema kwamba kazi hii haifuati kaida ya kijadi ya kuikita hadithi katika mandhari mahsusi ya kijamii. Hali hii tunaikuta pia katika *Mzingile*. Kimsingi, riwaya zote nne za awali alizozindika Kezilahabi zinahusu maisha ya Kitanzania na mandhari yake ni kisiwa cha Ukerewe. Katika *Nagona* na *Mzingile* tunaona kuwa mwandishi anamgurisha msomaji kutoka mazingira ya kiulimwengu aliyoyazoea, na kumpeleka kwenye ulimwengu wa kindoto baina ya kifo na uhai; baina ya kuwa macho na kuwa usingizini. Kwa kufanya hivyo, anamshirikisha msomaji katika safari ya kifikra ya kutalii ulimwengu ili kuujua ukweli wake. Safari hii inapindua kabisa mtazamo wa kikaida wa ulimwengu na maisha ya mwanadamu. Picha ya maisha tunayosawiriwa ni ya kutisha na isiyoleta matumaini yoyote.

Vipengele muhimu vya picha hiyo ni kama vifuatavyo:

1. Mwanadamu anajikuta katika ulimwengu nasibu ambapo kitu kinacholeta mabadiliko ni ajali. Hivi ni kumaanisha kwamba mwanadamu hana uwezo wa kuyaendesha na kuyapanga maisha yake. Hata kuwepo kwake ulimwenguni si kwa hiari yake bali ni matokeo ya ajali. Msimulizi katika *Nagona* anaambiwa: "Kuzaliwa kwenu ndiyo ajali kubwa iliyopata kutokea katika uhai wenu" (uk. 23). Vivyo hivyo, kuondoka ulimwenguni kwa mwanadamu hakutegemei hiari yake bali matokeo ya ajali.

2. Maisha ya mwanadamu hayana matilaba yoyote na ni batili. Wazo hili linakuzwa kikamilifu katika kazi zote mbili, hasa kwa kutumia taswira ya msafiri aliyepotea njia. Katika *Mzingile*, msimulizi anatumwa na walimwengu kwenda kumwambia Mungu kuwa wamemuua mwanawe, Mkombozi wa Pili. Lakini hata anapioanza safari - ambayo ni kiunzi cha kazi nzima, hajui aelekee wapi.

Anasema: "Sikujua nielekee upande gani maana hakuna aliyejua kwa hakika mahali alipoishi" (uk. 6). Ubatili wa maisha unatiliwa mkazo na sitiari ya *Mzingile*. *Mzingile* ni hali ya kutatanisha na kuudhi. Hii ndiyo hali anamojikuta mwanadamu maishani. Ni kama samaki aliyenaswa katika wavu, Anapatapa tu bila kuwa na uwezo wa kujiokoa. Juhudi zote za mwanadamu kujitoka katika "mzingile" wa kutojua ukweli wa maisha zinashindwa. Safari za wasimulizi katika kazi zote mbili ni za kimzunguko na hatimaye zinawarudisha walikotoka, bila kuwaletea matumaini yoyote. Katika novela ya *Mzingile*, tunapata picha ya mwanadamu kama kiumbe aliyezongwa kabisa na wazo la Mungu, hivi kwamba amekuwa mtumwa wake. Mhusika mkuu anamfokea Mungu akisema: "Mwongo mkubwa! Kila mahali niendako nakukuta! Wewe ndiye uliyenifanyia mazingaombwe niwe mtu wa kukufuata milele! Mimi si mtumwa wako, Nataka uhuru wangu sasa..." (uk. 58). Hatimaye, anashindwa kuupata uhuru wake. Anashindwa kulitoa wazo la Mungu katika mfumo wa fikira zake.

3. Mwanadamu hawezi kupata fanaka na furaha maishani mwake kwa sababu ulimwengu anamoishi ni mbovu na haumjali. Katika *Nagona* mwanamke anayebeba mimba ya Mkombozi wa Pili anasema "Ulimwengu tambara bovu. Ni vigumu kuubeba. Katika uhai wangu wote nimekuwa hapa nikijaribu kuubeba. Nachoka, nakoga, najaribu tena, na bado sijafanikiwa..." (uk. 24). Juhudi anazofanya mwanadamu ili kujiendeleza apate furaha, kumbe ni za kumlelea maangamizo. Viwanda anavyovijenga kufuatia uvumbuzi wa kisayansi vinautia sumu ulimwengu na kuleta maafa. Katika kazi zote mbili, hasa *Nagona*, msimulizi ambaye ni kiwakilishi cha mwanadamu aghalabu anaanza kusimulia visa vyake kwa kueleza mazingira aliyomo. Mara nyingi, mazingira haya yanakuwa ni bondeni. Dhana ya bonde inazua picha ya mahali palipotawaliwa na giza, ukungu, ukiwa na mauti. Bonde ni taashira ya ulimwengu ambayo inasisitiza kwamba ni mahali pasipofaa kwa kuishi. Katika fasihi ya uduni (*Literature of the Absurd*), suala la mandhari ni muhimu sana. Wasanii katika tapo hili, ambapo tunamweka Kezilahabi, hutumia mandhari kubainisha msimamo wao kwamba ulimwengu ni wa kinasibu, duni, na wa kukatisha tamaa. Katika kazi za Samuel Beckett, mwandishi mashuhuri wa tapo hili, tunakuta matumizi kama hayo ya mzingira. Kwa mfano, mazingira yanayotawala katika tamthilia yake *Waiting for Godot* ni ya gizagiza, yanayozua hisia za uchovu, huzuni na kukata tamaa. Estragon na Vladimir, wachusika wawili ambao ni wazururaji, wanamsubiri Godot ambaye hatokei. Hii ndiyo hali ya mwanadamu anayesubiri mafanikio na maisha bora ambayo hayaji. Taashira ya matarajio haya ni Mwokozi ambaye anaaminiwa na wengi kuwa atakuja kuleta neema.

4. Katika *Nagona* tunaonyeshwa kwamba, historia ya mwanadamu haina chochote cha kujivunia. Kwa karne nne zilizopita, maisha katika ulimwengu

yamekuwa vurumai tupu ambayo imesababisha maafa makubwa. Kwa karne mbili ambapo mfumo wa kibepari umetawala, uoza wa dunia umefikia kilele chake. Maafa yaliyoletwa na ubepari ni kama vile, mauaji ovyoovyo ya Watu Weusi na Wahindi wakati wa kuimarisha makoloni, ubaguzi wa rangi, ufilisishwaji wa nchi za Ulimwengu wa Tatu na mataifa makuu ya kibepari, na uangamizaji wa imani za kidini. Kadiri wakati unavyopita, karne hii ikielekea ukingoni, ndivyo vurumai itakavyozidi na maafa yake kuwa makubwa zaidi.

5. Dhana ya ukweli ndiyo ambayo imechukua nafasi kubwa zaidi katika picha ya maisha iliyosawiriwa katika kazi zote mbili. Ukweli, hususan kuhusu kuwepo kwa mwanadamu ulimwenguni ndilo fumbo kuu la maisha. Historia ya mwanadamu ni kama mfululizo wa jitihada za kulifumbua fumbo hilo. Kama tulivyogusia hapo juu, motifu ya msimulizi kusafiri kwenda kutafuta ukweli imekithiri hasa katika *Nagona*. Anakariri: "Daima nilitaka kupazuru pale ambapo kweli imedhihiri" (uk. 24). Katika novela hii, mwandishi ametumia sitiari tatu kufumbatia dhana ya ukweli. Sitiari hizo ni:

(a) **Mwanga:** Ukweli ni mwanga ulio katikati ya duara. Wanadamu huzunguka duara hii bila kufika katikati kwenye ukweli. Ni kama vile ambavyo wadudu huzunguka mwanga wa taa. Wakiukaribia sana mwanga huo, huungua. Vivyo hivyo, wanadamu hukumbwa na maafa mengi katika safari ya kuutafuta ukweli.

(b) **Paa:** Ukweli ni paa aliyekurupushwa na akapotea ulimwenguni karne nyingi zilizopita. Msimulizi anausiwa na babu yake kuwa wakati utafika ambapo atachukua uta na mishale kwenda kumsaka huyo paa. Anaposhindwa "kumjua" paa baada ya kumpata, hilo linaelezwa kama Anguko la Pili. Ni muhimu kulifafanua fumbo hili kwa sababu ndilo kiini cha ujumbe wa mwandishi. Tunaanza kwa kujiuliza anguko la Kwanza ni lipi? Katika Biblia na Qurani, anguko la mwanadamu linajitokeza katika hadithi ya Adamu na Hawa. Tunaambiwa kwamba Mungu alipoumba ulimwengu, aliwaumba Adamu na Hawa wakiwa wanadamu wa kwanza, na kuwaweka kwenye bustani ya Eden ambapo waliishi kwa furaha na kwa masikilizano mazuri na muumba wao. Walipotenda dhambi, masikilizano hayo yalivunjika, wakafukuzwa kutoka bustani hiyo, na maisha yao yakawa magumu. Dhambi yao ya kwanza na matokeo yake, ndicho chanzo cha masaiibu ya wanadamu mpaka hivi leo. Katika muktadha huu, anguko la Pili ni kushindwa kwa mwanadamu kwa mara ya pili katika mtihani wa kuyapa maisha yake maana na mwelekeo. Hivyo basi yanabakia batili na katili.

(c) **Nagona:** Nagona ni sitiari ya ukweli inayoziunga pamoja sitiari mbili zilizotajwa hapo juu. Kwanza, Nagona ni mwanga. Pili, Nagona ni msichana

mzuri, yaani paa ambaye msimulizi anampata baada ya kushinda mitihani mingi, lakini akashindwa katika mtihani wa mwisho wa kumshika na kumjamii. Sifa kuu ya sitiari zote tatu ni utelezi wake. Hivi ni kumaanisha kwamba ukweli ni dhana telezi, ambayo mwanadamu hana uwezo wa kuidhibiti. Kufichana kwa ukweli kunanasibishwa na kitendawili kigumu ambacho mwanadamu ametegewa na kiumbe mwovu aitwaye Sphinx.⁶

Hitimisho

Tumeona kwamba Kezilahabi ni mwandishi aliyevutiwa na masuala ya kifalsafa yanayovuka mipaka ya kitaifa na yanayowahusu wanadamu wote. Hata hivyo, masuala yoyote yale ya kifalsafa yaliwekwa katika muktadha wa kijamii na kihistoria. Hivyo basi, hatimaye Kezilahabi alijitokeza kama mwandishi wa kijamii aliyeihakiki jamii yake na kubainisha chanzo cha mikinzano yake. Mkondo huu wa uandishi unabadilika baada ya kutokea *Nagona* na *Mzingile*. Hizi ni kazi za kifalsafa zilizokolea udhanaishi na zinazomtoa mwandishi kutoka tapo la waandishi wakiuhalisia na kumkita katika tapo la fasihi ya uduni. Ni kutokana na mabadiliko haya ya kimwelekeo ambapo hata umbo la kazi zake linabadilika. Tayari tumegusia ugumu wa kuziainisha kazi zinazowakilisha mabadiliko hayo. Mhakiki wa fasihi ya uduni aghalabu hukumbwa na tatizo hilo. Tazito hutokea, kwa sababu kama anavyosema Benet (1965), fasihi ya uduni huwa imedhamiriwa kuvunja kaida za uandishi wa tanzu za kijadi kama riwaya na tamthilia, pamoja na kuzifanya zionekane kuwa za kuchekesha ili kubainisha uduni wa maisha ya mwanadamu⁷. Hivyo ndivyo Kezilahabi alivyofanya katika *Nagona* na *Mzingile*, ambapo anavuruga kimakusudi taratibu za utunzi wa riwaya.

Mabadiliko yanayojitokeza katika kipindi cha pili cha uandishi wa Kezilahabi yanaonyesha kwamba sasa amekuwa mfuasi mwaminifu wa falsafa na mienendo ya uandishi ya kimagharibi kuliko vile alivyokuwa awali. Falsafa ya udhanaishi anayoifuata ilizuka huko Ulaya katika mazingira mahsusi ya kijamii na kihistoria. Kimsingi ilizuka kama upinzani dhidi ya mwelekeo wa kifikra uliojulikana kama Enzi ya Mantiki (*the Age of Reason*). Waandishi wa fasihi ya uduni katika mataifa ya Ulaya waliathiriwa sana na falsafa ya udhanaishi kwa sababu mwelekeo wake uliafikiana na mazingira ya kijamii yaliyotawala wakati huo. Ilikuwa ni baada ya Vita Vikuu vya Pili. Vita hivyo vilisababisha uharibifu mkubwa wa amali na maisha kwa kiwango ambacho hakikuwahi kufikiwa katika historia ya mwanadamu kabla ya hapo. Vita vilivuruga kabisa jamii nyingi za kimagharibi. Hatukatai kwamba hata Afrika Mashariki iliathiriwa na vita hivyo. Lakini kimsingi vilikuwa ni vita baina ya mataifa makuu ya kibepari. Kwa hivyo Kezilahabi anapotumia falsafa ya udhanaishi katika uandishi wake, anajaribu kuwafanya wasomaji wake waathirike na tajiriba ya kihistoria ambayo waliishiriki kidogo tu. Ikiwa vita vilisababisha maafa katika mataifa ya kimagharibi

yanayohusika, basi waandishi wa kimagharibi wanaofuata mkondo wa udhanaishi wana haki ya kuomboleza kwa msiba huo katika fasihi yao ya uduni. Kwa hali hii, uandishi wa Kezilahabi unatushawishi kuulilia msiba usiokuwa wetu. Kwa nini uoza na uduni wa jamii za kimagharibi utushughulishe hali sisi tuna matatizo yetu ambayo tunapaswa kuyashughulikia. Kama mtunzi wa fasihi ya uduni, Kezilahabi anafaulu zaidi katika kipindi cha pili cha uandishi wake. Lakini tunasisitiza kwamba fasihi ya aina hii haielekei kuwa na umuhimu mkubwa katika mazingira ya Afrika Mashariki. Kwa sababu hii, *Nagona* na *Mzingile* zinaelekea kuukwamisha uandishi wa Kezilahabi badala ya kuuendeleza.

Tanbihi

- 1 Hadithi hizo zimechapishwa katika kitabu cha Mbunda Msokile: *Misingi ya hadithi Fupi*, Dar es Salaam University Press, 1982.
- 2 Taz. *Kiswahili*, Jarida la TUKI, Tol. 50/1, 1983, uk.1.
- 3 Taz. Kazi yake: *An Investigation of Themes in Swahili Literature and an Application of Stylostatistics to Chosen Texts*, tasnifu ya Ph.D, Nairobi, 1982, uk. 118.
- 4 S.A.K. Mlacha na J.S. Madumulla, *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam University Press, 1991, uk. 1.
- 5 Kwa kifupi, novela au riwaya sahili, ni kazi ya kubuni yenye urefu na utata wa wastani baina ya riwaya na hadithi fupi.
- 6 Katika visaasisli vya Kigiriki, Sphinx alikuwa kiumbe wa kutisha mwenye uwezo mkubwa maradufu kuliko mwanadamu. Kiumbe huyu alitumwa na miungu wa mji wa Thebes kuwategea wapita njia kitendawili kigumu kilichowashinda kutegua. Wote walioshindwa waliliwa naye.
- 7 Taz. W.R. Benet, *The Readers' Encyclopaedia*, London: Adam and Charles Black, 1965, uk. 4.

Marejeo

- Benet, W.R. (1965). *The Readers' Encyclopaedia*. London: Adam and Charles Black.
- Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- (1974). *Kichwamaji*. Nairobi: East Africa Publishing House.
- (1979). *Gamba la Nyoka*. Arusha: East African Publications Ltd.
- (1990). *Nagona*. Dar es salaam University Press.
- (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam University Press.
- Mlacha, S.A.K. na Madumulla, J.S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam University Press.
- Msokile, M. (1982). *Misingi ya Hadithi Fupi*, Dar es Salaam University Press.
- Mulokozi M.M. (1983). *Tahakiki: Dunia Uwanja wa Fujo katika Kiswahili 50/1*
Dar es Salaam: TUKI
- Topan, F. (1982). katika *Swahili Language and Society*. London: SOAS.